



MKOA WA SONGWE



FOMU YA USAJILI WA MBIO ZA RIADHA ZA KIMONDO MARATHON JUNI 28, 2018

Wanaoshiriki katika Mbio za Kimondo Marathon ikiwemo mbio fupi zote watambue kuwa tahadhari zote zimechukuliwa na waandaaji ili kuhakikisha usalama wa washiriki, ijapokuwa bado kuna uwezekano wa mshiriki kuumia/kupata jeraha katika



mashindano haya. Washiriki Kwa kutambua hilo wanashiriki kwa hiari yao wenyewe na endapo lolote litatokea hawatadai chochote kwa waandaaji, wadhamini, au mamlaka zozote za uandaaji wa mashindano haya. Wazazi na walezi watathibitisha ushiriki wa watoto wao kwa kuweka saini katika fomu hii ya usajili.

MAELEZO BINAFSI:

Jina la Ukoo.....

Jina la Kwanza.....

Majina Mengine.....

Uraia.....

Tarehe ya Kuzaliwa.....

Jinsia.....

Aina /Namba ya Kitambulisho...

Anuani.....

Namba ya Simu.....

Barua Pepe.....

| | | | | | |
|----|--|----|--|------|--|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| KE | | ME | | UMRI | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

Hakikisha unajisajili mapema, chagua mbio utakazo shiriki hapa chini:

Km 21 (HalfMarathon)

Km 5

Mita 100 mpaka 1500

Umri zaidi ya miaka 18

Watoto miaka 13-18

Watu wote

Zawadi kwa mbio ndefu za Km 21 ni kama ifuatavyo:

| NAFASI YA | WANAWAKE - Tsh | WANAUME-Tsh |
|-----------|----------------|-------------|
| Kwanza | 1,000,000/- | 1,000,000/- |
| Pili | 800,000/- | 800,000/- |
| Tatu | 500,000/- | 500,000/- |
| Nne | 300,000/- | 300,000/- |
| Tano | 250,000/- | 250,000/- |

Zawadi kwa ajili ya mbio fupi za kuanzia mita 100 mpaka 1500 zitaanzia shilingi elfu hamsini. Mbio za watoto za Kilomita tano zawadi zitaanzia shilingi laki moja. Mbio zote zitafanyika tarehe 28 Juni 2018 kuanzia saa 12.30 asubuhi, mbio za Km 21 zitaanzia uwanja wa CCM Vwawa-Mbozimpaka uwanja wa Kijiji cha Ndolezi-Mbozi aidha mbio nyingine zitafanyika katika uwanja wa Kijiji cha Ndolezi. Fomu za usajili zinapatikana Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe zilizopo eneo la Bomani Vwawa-Mbozi. Kwa malipo ya usajili tumia namba 0744-175-056 au 0719-475-480 na Akaunti. Na. 61210011744 NMB-MBOZI RAS SONGWE IMPREST Kisha ulete paying slip/nakala ya malipo, gharama za malipo ya usajili ni sh. 10,000/-

- NB:**
1. Jina ulilolipia liwe sawa na jina ulilosajilia kwenye fomu
 2. Hakikisha pesa unalipia kwenye Akaunti na namba za simu zilizopo hapo juu siyo kutoa pesa mkononi.
 3. Mara baada ya kufanya malipo hakikisha unatuma ujumbe mfupi wa jina lako kamili na muamala umefanya wa aina gani (mpesa, tigopesa au bank) ili uweze kuwekwa kwenye orodha ya washiriki.

Kwa maelezo zaidi tumia namba hapo juu au tembelea tovuti ya www.songwe.go.tz utapata fomu kwenye kipengele cha machapisho.

KUMBUKA

Unaposaini fomu hii hapo chini unathibitisha kuwa umeelewa na unakubaliana na masharti yote na vigezo vilivyowekwa. Pia unaidhinisha kutumika kwa jina, sauti na picha (mnato na video) zako katika televisheni, redio, matangazo, promosheni au kwa namna yoyote ambayo waandaji na wadhamini watataka.

Sahihi ya mshiriki:

Jina na Sahihi ya Mzazi au Mlezi kwa watoto chini ya Miaka 18:


K. N. Y. KATIBU TAWALA
SONGWE